

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO



TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

**YAH: UTEUZI WA MWENYEKITI WA BODI YA WAKURUGENZI YA
KILIMANJARO AIRPORTS DEVELOPMENT COMPANY (KADCO)**

Nimepewa taarifa na Mhe. Waziri mwenye dhamana ya Sekta ya Uchukuzi kwamba, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli ametengua uteuzi wa Mwenyekiti wa Bodi ya Kilimanjaro Airports Development Company (KADCO), **Balozi, Hassan O. Gumbo Kibelloh.**

Kufuatia hatua hiyo Mhe. Rais amemteua **Bw. Gregory George Teu** kuwa **Mwenyekiti wa Bodi ya KADCO** kwa mujibu wa Sheria ya "The Public Corporations Act" [Cap 257 R.E.2002] kifungu cha 9 (1) na (2). Uteuzi huu unanza tarehe **16/10/2017.**

Aidha, Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano Mhe. Prof. Makame Mbarawa (Mb) ametengua uteuzi wa Mjumbe wa Bodi hiyo **Bw. Suleiman Suleiman** kuanzia tarehe 16 Oktoba, 2017.

A handwritten signature in blue ink, appearing to read 'Leonard M. Chamuriho'.

Dkt. Leonard M. Chamuriho
KATIBU MKUU - UCHUKUZI

16/10/2017